



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI



04/06/2022

TANGAZO

UWAKALA WA USAFI WA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali inakaribisha maombi ya kuwa wakala wa Usafi wa Mazingira ya Halmashauri kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 kutoka kwa wazabuni wenye sifa za kufanya kazi hiyo kwa maeneo yafuatayo;-

1. LGA/076/US/2022/2023/01 – Huduma ya Uzoaji na Ukusanyaji taka ngumu Kata ya Chimala
2. LGA/076/US/2022/2023/02 – Huduma ya Uzoaji na Ukusanyaji taka ngumu Kata ya Igurusi
3. LGA/076/US/2022/2023/03 – Huduma ya Uzoaji na Ukusanyaji taka ngumu Kata ya Lugelele
4. LGA/076/US/2022/2023/04 – Huduma ya Uzoaji na Ukusanyaji taka ngumu Kata ya Ubaruku
5. LGA/076/US/2022/2023/05 – Huduma ya Uzoaji na Ukusanyaji taka ngumu Kata ya Rujewa
6. LGA/076/US/2022/2023/06 – Huduma ya Uzoaji na Ukusanyaji taka ngumu Kata ya Madibira


MASHARTI YA MAOMBI

1. Mwombaji awe na leseni hai ya biashara, TIN, Hati ya usajili, Utambulisho wa kisheria (Power of Attorney) na pia awe na ofisi inayotambulika (Ataje Ofisi ilipo, Anwani, Namba ya simu, Email na Fax kwa ajili ya mawasiliano).
2. Mwombaji awe na vitendea kazi kama vile gari, trekta au guta kwa ajili ya kufanya kazi ya usafi.
3. Mwombaji awe tayari kutumia viwango vilivyowekwa na Halmashauri na atumie sheria ndogo ya Usafi wa Mazingira.
4. Mzabuni atatumia mfumo wa kielektroniki kukusanyia mapato ya ndani ya Halmashauri.
5. Mzabuni atatakiwa kuwasilisha makusanyo yote ya siku kwenye akaunti ya mapato ya ndani ya Halmashauri.
6. Waombaji wanaweza kuwa Makampuni, Mashirika au Vikundi vya watu waliosajiliwa kisheria.
7. Mwombaji asiwe na deni lolote analodaiwa na Halmashauri ya Wilaya Mbarali.
8. Mwombaji haruhusiwi kuweka alama yoyote ya utambulisho wake juu ya bahasha.
9. Mwombaji aambatanishe idadi ya kazi alizowahi kufanya Serikalini au kwenye Taasisi zinazotambulika hapa Nchini, ikiwa na vielelezo (barua ya kuteuliwa kuwa wakala, mkataba wa kazi), uwezo wa kifedha (financial Capacity – Bank Statement ya miezi mitatu ya Machi, Aprili na Mei 2022).

10. Mwombaji ataruhusiwa kuomba zaidi ya zabuni moja kwa kutumia maombi kwenye bahasha tofauti. Juu ya bahasha iandikwe **HERUFI KUBWA** namba ya zabuni aliyoomba, aina ya zabuni, na ifungwe kwa **LAKIRI (Seal)** na maombi yakiambatana na kivuli cha stakabadi ya ada ya maombi yaletwe/yatumwe kwa;

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI,
S. L. P 237,
RUJEW – MBEYA.**

11. Vitabu vya zabuni kwa lugha ya kiswahili vinauzwa kwa **Tshs. 100,000/=** ambazo hazitarudishwa kwa mwombaji na vinapatikana katika ofisi ya Afisa Ugavi (W), **Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, S. L. P 237, RUJEW – MBARALI.**
12. Malipo yafanyike kupitia **Benki ya NMB**, Akaunti ya **Own Source Collection**, Akaunti namba **6110000719** na slip ya bank iletwe kwa mhasibu ili kupatiwa risiti kuanzia saa 02:00 asubuhi hadi saa 09:30 alasiri siku za kazi.
13. Maelezo ya ziada (masharti) yanapatikana kwenye kitabu cha zabuni husika.
14. Bodi ya zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali hailazimiki kukubali au kukataa ombi lolote.
15. Mwombaji anashauriwa kabla ya kuomba zabuni yoyote kufanya utafiti wa kutosha.
16. Mwombaji anaweza kuja ofisi za Halmashauri kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kupata ufafanuzi atakaohitaji ikiwa ni pamoja na kuonyeshwa sehemu za kukusanyia taka.
17. Mwisho wa kuwasilisha maombi ni 14/06/2022 saa 5:00 asubuhi na zabuni zitafunguliwa siku hiyo saa 5:01 asubuhi katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya. Waombaji au wawakilishi wao wanakaribishwa kuhudhuria siku ya ufunguzi.



.....
Missana K. Kwangura,
Mkurugenzi Mtendaji (W)
MBARALI

